RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA MIFUGO, UTALII, UWEZESHAJI NA HABARI YA
BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR, KATIKA KUFUATILIA UTENDAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

TANZIA

Awali ya yote, Kamati inaungana na Kamati zote katika kumkumbukuka na kumuombea Dua njema, Mwezetu Marehemu Salmin Awadh Salmin aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni . Marehemu ambae mbali na mchango wa ujumla ndani na nje ya Baraza la Wawakilishi, pia aliisaidia sana Kamati hii kwa michngo yake ya busara na tija wakati tulipomwalika katika vikao vyetu mbali mbali, na pia ushauri wake mzuri wakati wote Kamati hii ilipohitaji mawazo yake. Kwa kweli Baraza la Wawakilishi tumempoteza mtu muhimu ambae alikua akitetea vyema kitu anachokiamini. Mungu azidi kumjaalia kheri na malazi mema Poponi, huku tukiamini kwamba yeye ametangulia tu nasi iko siku tutafuatia.

SEHEMU YA KWANZA:

UTANGULIZI

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kama Kamati nyengine za Baraza la Wawakilishi imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na imeundwa kwa mujibu Kanuni ya 106(i) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi , Toleo la 2012 . Aidha Kanuni ya 115 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi inabainisha na kufafanuwa Kazi na majukumu ya Kamati hii.

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ambapo katika ripoti hii inajulikana kama " Kamati", inawajibu wa kufuatilia utekelezaji wa wizara mbili za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar , ikiwa ni pamoja na Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni kama zifuatazo:-

1) Wizara ya Habari,Utamaduni , Utalii na Michezo; na
2) Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Pamoja na mambo mengine Kamati imepewa majuku yafuatayo:-

a) Kufuatilia Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotowa katika Baraza.
c) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
f) Kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika.
g) Kuchambua ahadi zote za wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo.
h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

WAJUMBE WA KAMATI

Kamati hii ina Wajumbe wanane na Makatibu wawili ambao ni :-

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-	Mwenyekiti.
2. Mhe. Abdullah Mohammed Ali	-	Makamo Mwenyekit
3. Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5. Mhe. Amina Idd Mabrouk	-	Mjumbe
6. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali	-	Mjumbe
7. Mhe. Asaa Othman Hamad	-	Mjumbe
8. Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
9. Ndg. Himid Haji Choko	-	Katibu
10. Ndg . Salum Khamis Rashid	-	Katibu.

MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa Mujibu wa Kanuni ya 108 (8) Kamati ilifanya kazi zake kwa utartibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa shabaha na malengo ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii na baadae kukagua baadhi ya Maeneo na taasisi za wizara hizo ili kuona maendeleo yaliyofikiwa. Kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015 Kamati ilifanyakazi kwa muda wa wiki sita (6) kati ya Unguja na Pemba kama ifuatavyo;

a) Unguja kuanzia 10/07/2014 hadi Jumatano ya tarehe 23/07/2014
b) Pemba kuanzia tarehe 08/12/2014 hadi tarehe 19/12/2014
c) Unguja kuanzia tarehe 02/2/2015 hadi tarehe 13/2/2015.

Hata hivyo kabla ya kuanza mwaka huu wa Fedha, Kamati yetu ilifanyi kazi kwa muda wa wiki mbili (2) hapa Unguja kuaanzia tarehe 30/12/2013 hadi Ijumaa ya tarehe 10/01/2014

HADIDU REJEA

Kamati ilifanya kazi zake kwa kutumia Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la Mwaka 2012, Hansard za Baraza za mwaka 2013/2014, Ripoti ya Kamati ya Mwaka 2013/2014 pamoja na Vitabu vya Hotuba za Bajeti za Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi vya mwaka 2014/2015

SEHEMU YA PILI.

A. WIZARA YA HABARI , UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari , Utamaduni, Utalii na Michezo ambayo ina dhamana ya kusimamia sekta kuu nne (4) ambazo ni Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ambapo ndani ya Wizara kuna Kamisheni mbili(2), Idara nne (4) , Tume Moja , Mabaraza Matatu (3) , Bodi moja (1) , Hoteli (1), Kamapuni moja (1) , Mashirika Mawili (2), Vyuo viwili (2), na Ofisi Kuu Pemba. Taasisi hizo ni kama zifuatazo;-

A. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
B. Idara ya Mipango , Sera na Utafiti,
C. Shirika la Utangazaji Zanzibar,
D. Idara ya Habari Maelezo,
E. Shirika la Magazeti ya Serikali,
F. Chuo cha Uandishi wa Habari,
G. Tume ya Utangazaji Zanzibar,
H. Kamapuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX),
I. Kamisheni ya Utalii,
J. Chuo cha Maendeleo ya Utalii,
K. Hoteli ya Bwawani,
L. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo,
M. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale,
N. Baraza la Kiswahili,
O. Baraza la Sanaa,
P. Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonyesho,
Q. Baraza la Taifa la Michezo,
R. Kituo cha EACROTANAL,
S. Ofisi Kuu Pemba.

SEKTA YA HABARI

Katika Sekta ya Habari, Kamati inaendelea kusikitishwa na mazingira magumu ya kazi licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na watendaji waliomo katika sekta hii. Hali hii inapelekea kuwepo na mafanikio kidogo yenye kutia Matumaini. Hata hivyo Sekta hii bado inakabiliwa na Changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi ili malengo yaliyowekwa na Wizara hii yaweze kufikiwa.

1. **Changamoto ya Kihabari Kisiwani Pemba.**

   Wakati wa kazi za Kamati, Kamati yetu ilifika kisiwani Pemba, ambapo ilitembelea taasisi mbali mbali ziliopo Chini ya Ofisi kuu Pemba. Katika ziara hizo Kamati imegundua kwamba, kuna **Changamoto kubwa ya kihabari Kisiwani Pemba**. Kamati imebaini Utamaduni wa woga na usiri mkubwa miongoni mwa viongozi wa serikali hasa Maofisa wadhamini katika utowaji wa habari au taarifa mbali mbali zenye maslahi kwa jamii kwa kisingizio kuwa hawaruhusiwi kutoa taarifa mpaka wapate idhini kwa

Makatibu Wakuu wao. Hali hii inaleta mvutano mkubwa kati ya wanahabari na baadhi ya Maafisa Wadhamini huko Pemba.

Maagizo na Ushauri wa Kamati

- Tatizo la Upatikanaji wa Habari kisiwani Pemba lipatiwe ufumbuzi kwani linakwenda kinyume na haki za Binadamu na Utawala bora. Aidha hali hii kama haitoangaliwa ipasavyo inaweza kuleta Chuki kati ya Vyombo vya habari, Serikali na wananchi.

- Wizara izishajihishe taasisi mbali mbali na viongozi kufanya ziara za makusudi na kuzungumza na waandishi wa habari katika Vilabu vyao na sehemu zao za kazi ikiwa ni njia moja wapo ya kujenga umoja na kuaminiana miongoni mwao.

2. **Mazingira Magumu ya Kazi Ofisi Kuu Pemba.**

Licha ya taasisi hizo zote ziliomo ndani ya jengo la Wizara ya Ya Habari, Utamaduni na Utalii Ofisi kuu Pemba kuendelea na majukumu yao kwa njia ya kizalendo, bado zinakabiliwa na Changamoto kadhaa kama ifuatavyo;-

(1) Uhaba wa vitendea kazi, ikiwemo Usafiri .
(2) Ufinyu wa Nafasi kwa taasisi zote ziliomo katika jengo hili ikiwemo Osifi ya Afsa Mdhamini mwenyewe.
(3) Mashirikiano madogo kati ya taasisi za Habari na Osifi nyengine hasa upatikanaji wa habari zinazohusu sehemu zao za kazi.

Ushauri na Maagizo ya Kamati.

- Kamati inaishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kuzipatia ufumbuzi wa haraka changamoto hizo ili vijana wetu wanaoendelea kujitolea kuchapa kazi ndani ya jengo la Ofisi hiyo kwa moyo wa kizalendo, wasivunyike moyo badala yake waimarishiwe mazingira yao ya kazi ili wazidi kulitumikia ipasavyo taifa letu.

3. **Vyama /Vilabu vya Waandishi wa Habari.**

Katika kuhakikisha kua tathnia ya Habari hapa Zanzibar inaimarika, waandishi wa Habari wameamua kujikusanya kwa pamoja na kuunganisha nguvu zao kwa kuunda vyama na vilabu mbali mbali. Wakati wa kazi za Kamati , Kamati yetu ilitembelea vyama hivyo ikiwemo Pemba Press Club iliyopo Chake chake , Baraza la Habari Tanzania (MCT) Ofisi ya Zanzibar iliyopo Mlandege na Jumuiya ya Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar iliyoko Mombasa.

Kamati imegundua kwamba vilabu na Vyama hivyo zimeanzishwa kwa lengo la kukuza viwango vya taaluma ya uandishi wa Habari kwa wanachama wake na kuraghibisha mashirikiano miongoni mwa waandishi wa habari, vyanzo vya habari na jumuiya za kitaaluma.

Aidha Vilabu hivyo viko mstari wa mbele katika kuhakikikisha kwamba Uhuru na haki ya kupata habari unalindwa, waandishi wa habari wanatekeleza vyema Wajibu wao (maadili) pamoja na Kufuatilia utendaji wa Vyombo vya habari.

Mafanikio ya Vilabu hivyo:-

- Kutoa mafunzo mbali mbali kwa wanahabari hapa nchini.
- Kuwaunganisha wanahabari hapa nchini kwa kuwa na sauti moja.

Maagizo na Ushauri wa Kamati

- Kutokana na juhudi na mchango mkubwa wa Vilabu vya waandishi wa Habari hapa nchini kwa wanachama wake , Kamati inaitaka Wizara kuongeza mashirikiano na vilabu hivyo.
- Kamati inaiomba Wizara Kukaa na wadau wengine ili kuzipitia upya sheria kandamizi dhidi ya uhuru wa habari ikiwemo Sheria ya Magazeti Namba 6 ya mwaka 1976 na Sheria ya Usalama wa taifa ya mwaka 1970 na nyengezo.

4. **Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)**

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) ni mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambalo limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria namba nne (4) ya mwaka 2013. Kamati inaamini kwamba Serikali ilikua na nia njema ya kuanzisha shirika hili kwa kuziuunganisha iiyokuwa Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) na Televisheni Zanzibar (TVZ) lengo likiwa ni kuwa na chombo kimoja chenye nguvu katika kuwahamasisha wananchi, kuwaelimisha na kuwapatia habari zilizofanyiwa utafiti, uhariri makini na zenye kuelezea sera na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kuhakikisha kwamba umoja wa wananchi wa Zanzibar unaendelea kudumu nchini.

Hata hivyo utendaji wa Shirika hili hivi sasa unapigiwa kilele, na wananchi hawaonyeshi kuridhika na utendaji huo. Kamati yangu imebaini kwamba ucheleweshaji wa Ruzuku kutoka Wizara ya Fedha, kunachangia kutokutekelezwa kikamilifu na kwa wakati Mipango ya Shirika hilo. Hapa Kamati inakubaliana kabisa na ile Nukuu isemayo “ **"Kama tunataka kupata maziwa bora, lazima tuhakikishe kuwa ng'ombe wetu tunampa malisho ya kutosha na kwa wakati”.**

Changamoto za Shirika.

(1) Kamati imebaini kuwa Shirika la ZBC lilianzishwa bila ya kuwa na msingi wa kutosha wa kujiendesha lenyewe, halikadhalika Shirika limerithi mzigo mkubwa sana wa madeni jambo ambalo linarudisha nyuma utendaji kazi wa Shirika.

(2) Shirika pia limerithi wafanyakazi wengi kiasi cha kupoteza dhana nzima ya kuitwa Shirika, suala ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kudhoofisha utendaji na uwajibikaji miongoni mwa wafanyakazi na watumishi.

(3) Sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Habari la Zanzibar ya Mwaka 2013, kifungu cha 20 kinamtaka Waziri atunge Kanuni baada ya kushauriwa na Bodi, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya vifungu utekelezaji wake unahitaji kutungiwa kanuni, lakini mpaka sasa hivi bodi haijamshauri Waziri kuhusiana na utungaji wa Kanuni hizo.

(4) Licha ya Kamati Kuipongeza ZBC kwa kuweka mitambo mipya na ya kisasa katika kituo chake cha TV Mkanjumi Pemba. Kamati inawasiwasi wa kudumu kwa muda Mrefu vifaa hivyo, kutokana na kwamba nishati ya umeme katika sehemu hiyo sio ya uhakika na upatikanaji wa Mafuta kwa ajili ya Standby Genarator ni tatizo.

(5) Bado taasisi nyingi za serikali, ikiwemo Baraza la Wawakilishi hazilipii baadhi ya matangazo yao, suala hili linarejesha nyuma ukusanyi wa mapato na hivyo kushindwa kujiendesha kama Shirika

Ushauri na Maagizo ya Kamati

- Kamati inaishauri Serikali inapoamuwa kuanzisha mashirika ijipange vizuri kwa kuyapa nyenzo na mtaji ya kutosha ili Mashirika hayo yawe na nguvu za kujiendesha yenyewe.
- Kamati tunaiagiza Wizara ya Habari , Utamaduni, Utalii na Michezo kukaa pamoja na Wizara ya Fedha kuangalia ufumbuzi wa madeni ambayo ZBC imerithi kutoka TVZ na STZ.
- Kamati inaishauri Bodi ya ZBC kumshauri Waziri kutunga Kanuni ili Sheria ya kuanzishwa kwa ZBC iweze kutekelezeka vizuri.
- Kwa mara nyengine tena Kamati inaitaka Wizara kukaa pamoja na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Wizara ya Fedha kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala la kulipia matangazo ya Mikutano ya Baraza la Wawakilishi kwa ZBC kwani kamati inaamini kua ZBC inaweza kujiimarisha sana endapo BLW litalipia matangazo hayo.
- Kamati inaishauri ZBC ibadilike na iendane na wakati ili iweze kuingia katika ushindani wa kibiashara na vyombe vyengine vya Habari.

5. Kampuni ya Zanzibar Multiplex (ZMUX)

Kamati imebaini kuwa lengo la kuanzishwa kwa Kampuni ya Zanzibar Multiplex (ZMUX) halijafikiwa, ikizingatiwa kwamba ZMUX imeanzishwa kama Kampuni ambayo ipo ndani ya Wizara ya Habari, lakini bado haijakuwa na vyanzo vya kukusanya mapato na kujiendesha yenyewe hivyo kuibebesha mzigo sana Serikali. Ni wazi kwamba lengo la kuanzishwa kwa Kampuni hii halijafanikiwa, na utafiti unaonesha kuwa nchi nyingi Taasisi zinazofanana na ZMUX huwa zinakuwa chini ya Shirika la Habari la Taifa la Nchi husika.

Ushauri na Maagizo ya Kamati

- Kamati inaiagiza Wizara kwamba Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kutafiti kuendelea kuwepo kwa ZMUX au la, ikamilishe kazi yake haraka na itowe majibu ya matokeo ya utafiti wao kwa wakati uliopangwa.

5. Shirika la Magazeti ya Serikali

Shirika la Magazeti ya Serikali limekuwa likichapisha magazeti yake ya kila siku ya "Zanzibar leo" na kila wiki "Zanzibar leo Jumapili" na "Zaspoti" ingawa linaendelea kujibana Katika jengo la ZBC, Redio Rahaleo mjini Zanzibar, Wakati Kamati inatembelea Ofisi za Shirika hilo, Kamati iligundua kwamba Shirika limeweza kuchapisha magazeti kama ilivyopangwa na kuyasambaza katika maeneo mbali mbali ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara huku likiendelea kufaidika na ufadhili wa Mfuko wa vyombo vya Habari Tanzania (TMF) ambapo Ofisi ya Pemba inaonekana kufaidika zaidi na Mfuko huo.

Changamoto za Shirika

- Mazingira ya kazi katika ofisi za Shirika hilo sio rafiki kwa utendaji wa kazi na kuna madai ya wafanyakazi kuathirika kwa ugonjwa wa presha na macho kutokana na hali ya joto na giza katika sehemu hizo.
- Kamati pia imegundua kwamba ukosefu wa fedha ni kikwazo cha kukiendeleza kiwanja kilichokusudiwa kujengwa Ofisi na Kiwanda cha magazeti ya Shirika hilo huko Tunguu.
- Kutokana na kukosekana kwa Mitambo ya kuchapishia magazeti ya rangi Zanzibar, shirika linaendelea kutumia fedha nyingi kwa gharama za uchapishaji wa magazeti huko Dar es salaam jambo ambalo linapelekea mzigo mkubwa wa gharama kwa Shirika.
- Wakati taasisi zilizo nnje ya Serikali zikiendelea kupunguza madeni yake , bado taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinadaiwa karibu shilingi milioni 400 kati ya shilingi 686,439,474/= zilizokuwa zikidaiwa kwa taasisi mbali mbali hadi kufikia Disemba 31, 2014.

Maagizo na Ushauri wa Kamati

- Kamati inazidi kushari kwamba Mradi wa Ujenzi wa Ofisi na Kiwanda cha Kuchapishia Magazeti ya rangi uingizwe katika Miradi ya Maendeleo katika Bajeti kuu ya Serikali.
- Kamati inaishauri Serikali kuwa, kuweko na utaratibu wa kuzilazimisha Taasisi za Serikali kupeleka matangazo yao katika Shirika la Magezeti la Serikali na walipie kwa muda ili Shirika lizidi kuimarika.
- Kamati inaishauri Wizara iwasiliane na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba wadaiwa wote walio chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakakatwa moja kwa moja kupitia katika vifungu vyao na kulipwa Shirika.

6. Kituo cha Redio Jamii- Tumbatu FM

Kamati inaendelea kuipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Shirika la UNESCO kwa kuendelea kuwahamasisha wanajamii kuazisha vituo vya Redio jamii. Kamati inaendelea kuamini kwamba vituo kama hivi ni muhimu, ambapo utafiti uanaonyesha kwamba jamii kadhaa ulimwenguni zenye vituo kama hivi zimepata maendeleo makubwa kupitia vituo vyao. Kutokana na Mwamko huo Redio Jamii nyengine mbili zimezinduliwa ikiwemo Redio Tumbatu na Redio Jamii Mkoani. Wakati wa kazi za Kamati Kamati yetu ilivuka Maji hadi Tumbatu kuangalia maendeleo ya redio hiyo.

Changamoto.

- Ushirikiano wa wanajamii katika kuhakikisha kuwa redio hizi zinaendelea kufanya kazi bado ni mdogo, ambapo wengi wao wanaamini kuwa wanaosimamia radio hizi huwa wanapata ufadhili mkubwa kutoka katika mataifa ya nje.
- Ofisi zao zipo ndani ya jengo la Ofisi ya Wilaya Ndogo ya Tumbatu, Kamati inaamini kwamba jambo hili linaweza kuifanya redio hii kufanya kazi kwa kufuata maelekezo ya mtu Fulani au kikundi Fulani suala ambalo ni kinyume na uanzishwaji wa radio hio.

Ushauri na Maoni ya Kamati

- Wizara izidi kutoa elimu juu ya madhumuni ya Kuazishwa vituo hivi vya redio na kwamba zimeitwa radio jamii kwasababu watakao endesha radio hizi sio serikali wala mataifa ya nje bali ni wana jamii wenyewe.

- Kamati inashauri Wizara kupitia nguvu za wanajamii ya Tumbatu kufanya kila litakalowezekana ili kituo hichi kipate ofisi yake ya kudumu ili iweze kufanya kazi zake kuwa uhuru na bila ya kuingilia na mtu yeyote.

7. Ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari

Kamati imeridhishwa na harakati za ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar hapo Kilimani. Shughuli hizo ambazo zimeanza Mwezi Desemba 2014 zinaonekana kutia matumaini na Kamati inaamini kwamba ujenzi huu utakapokamilika kutasaidia sana katika kupunguza tatizo la uhaba wa madarasa ya kufundishia katika chuo hiki.

Changamoto

- Uhaba wa vifaa vya Ujenzi unaotokana na uhaba wa Bajeti.
- Chuo hakina hati miliki ya eneo hilo.

Maagizo ya Kamati

- Wizara itafute Hatimiliki ya eneo hilo ili liendelee kuwepo kwenye usalama zaidi na kujiepusha na khitilafu zozote zinazoweza kujitokeza katika suala la umiliki.
- Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuwapatia fedha za ujenzi kwa wakati ili ujenzi huo umalizike kwa haraka.

SEKTA YA UTALI

Sekta ya Utalii inahusisha taasisi tatu ambazo ni Kamisheni ya Utalii, Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Hoteli ya Bwawani.

8. Kituo cha Kukusanya Habari Na Takwimu Za Utalii

Kamati ilipata fursa ya kutembelea vituo vya kukusanya Habari na takwimu za watalii Uwanja wa Ndege Kisauni, na Bandanirini Malindi Mjini Zanzibar. Kamati inapongeza kuazishwa kwa vituo hivi kwani inaamini kwamba Takwimu zinazokusanywa zinasaidia katika kuweka kumbukumbuku nzuri ya uingiaji wa Watalii Zanzibar lakini pia inasaidia katika kuweka kumbukumbu za ukusanyaji mapato yanayotokana na Utalii.

Kamati ilipofanya ziara katika vituo hivyo imebaini kwamba wanaokusanya taarifa hizi ni maafisa kutoka idara ya Uhamiaji na baadae wanazipeleka katika vituo hivyo kwa ajili ya kujaza taarifa hizo, vituo hivyo vimejumuisha wafanyakazi kutoka katika Afisi ya Mtakwimu mkuu wa Serikali na Kamesheni ya Utalii.

Kwa kuwa Utalii ni moja ya vyanzo vikuu vinavyoingiza mapato hapa Zanzibar, kamati inaendelea kusisitiza juu ya kuimarishwa kwa vituo hivyo.

Changamoto

Vituo hivi vinakabiliwa na Changamoto zifuatazo:

(1) Vituo vinakabiliwa na tatizo la uhaba wa nafasi, katika osifi za vituo hivyo kulingana na kazi wanazozifanya.

(2) Uhaba wa vitendea kazi.

Maagizo na ushauri wa Kamati

- Serikali ifanye jitihada za kuwapatia eneo la kuridhisha wafanyakazi waliopo eneo la Uwanja wa Ndege, kwani eneo la uwanja wa ndege ndio ambalo asilimia kubwa sana ya watalii wanapoingia, kwahivyo kuendelea kutumia Afisi iliyopo hivi sasa ni kuudhalilisha utalii Zanzibar.

- Wizara ihakikishe kwamba wafanya kazi wa vituo hivyo wanakuwa na vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa.

- Kwakuwa, katika hatua za awali, Afisi ya Uhamiaji ndio inayokusanya taarifa, Kamat inashauri kuwa wakati wa kupokea taarifa hizo awepo pia na mtumishi kutoka kituo cha kukusanya habari na takwimu za watalii.

9. Chumba cha Chini kwa Chini - Makangale

Kamati ilifika huko Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Mradi wa Hoteli ya Kitalii Manta Resort. Kamati ilitembelea mradi maarufu wa chumba Cha chini kwa chini kiliopo chini ya bahari katika hoteli hiyo ambacho kimekua ni kivutio kikubwa cha watalii. Kamati imegundua kwamba Chumba hicho ni miongoni mwa vivutio Vikubwa vya sehemu za Kitalii hapa Zanzibar

Changamoto yenye kuleta Matumaini.

- Meneja wa hoteli hiyo ameijulisha Kamati kwamba wageni wengi wanaotembelea Chumba hicho wamekuwa wakilalamika kwamba wamekuwa wakiilipia chumba hicho siku nzima lakini kwa furaha, huwa wanashindwa kupata usingizi kutokana na vivutio mbali mbali ikiwemo samaki, matumbawe na mazao mengine ya baharini hasa wakati wa usiku.

Maagizo ya Kamati

- Serikali iimarishe miundombinu ya barabara na maji katika hoteli hizo ili eneo hilo lifikiwe kwa urahisi.
- Wizara ikishirikiana na Muwekazeji huyo iendelee kukutangaza Chumba hicho duniani kote.

10. Hoteli ya Bwawani.

Hoteli ya Bwawani ni miongoni mwa taasisi za Serikali iliyo chini ya WHUUM na ni miongoni mwa matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 yaliyoachwa na muasisi wa Mapinduzi hayo Marehemu Mzee Abeid Aman Karume. Kamati imebaini kuwa bado kuna tatizo la baadhi ya Taasisi zinazokodi ndani ya Hoteli ya Bwawani kutokulipa kodi zao.

Licha ya hatua iliyochukuliwa na Uongozi wa Hoteli ya kuzifungia Taasisi hizo ambazo hazijalipa lakini bado Kamati inaendelea kusisitiza kuwa wadaiwa hawa wafunguliwe kesi Mahkamani haraka iwezekanavyo, na kuchekelewa kufanya hivyo tunaweza kupoteza haki za hoteli kwani , kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo " Limitation Act" madai yote yana muda wake maalum, na muda huo ukipita hutaweza tena kufungua dai hilo mbele ya Mahkamani.

Maagizo na Ushauri wa Kamati.

- Wizara izidi kufutilia madeni yote ya Hoteli hiyo na kuhakikisha kwamba wadaiwa wote wanakumbushwa .
- Wizara iwachukulie hatua za kisheria wadaiwa sugu waliopanga hoteli ya Bwawani.

SEKTA YA UTAMADUNI NA MICHEZO

11. Mgogoro ndani ya Chama Cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA)

12.

Kamati ilikutana na Uongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFA) na kupokea taarifa ya utendaji wa Chama hicho. Kamati imesikitishwa sana kuwa ZFA imepoteza kabisa mwelekeo wake na kimeshindwa kutekeleza majukumu yake, hii inatokana na migogoro iliyopo kwa viongozi wao wenyewe kutokufahamiana, jambo ambalo limepelekea kutokufanya kazi zao kwa mashirikiano na kugawika makundi mengine ndani ya ZFA ambayo yanapingana na kundi jengine miongoni mwao.

Matokeo ya Mgogoro huo

Kamati inaendelea kusikitishwa kutokana na kukua kwa mgogoro huo hadi kufikia hatua ya kusimama kwa ligi kuu ya Zanzibar jambo ambalo linapelekea kuondosha heshima ya Soka ya Zanzibar . Aidha pande zinazovutana zimeendelea kuukuza mgogoro huo hadi kuburuzana Mahakamani , na hadi Kamati inataayarisha Ripoti hii liko mahakamani .

Maoni ya Kamati.

1. Kamati isingependa kulizungumzia sana suala hili ispokuwa ni kuishauri wizara kutumia hekima na busara kuzikutanisha pande zinazovutana ili walimalize suala hili nnje ya Mahakama.

2. Kuendelea kuwepo kwa mgogoro huu ni kudumaza Mchezo wa Soka hapa Zanzibar.

B. WIZARA YA MIGUFO NA UVUVI

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni miongoni mwa wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo Kamati inatambua kwamba Wizara hiyo inalenga kuongeza ajira , Pato la Taifa, lishe bora na kupunguza umasikini kwa wananchi na kuwepo uhakika wa chakula kwa kila kaya hapa nchini.

Wakati wa kazi za kamati ndani ya Wizara hiyo, Kamati iligundua kwamba Malengo hayo yanatekelewa ndani ya majukumu ya wizara hayo kupitia Idara zake sita na Afisi Kuu Pemba. Kama ifuatavyo:-

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
3. Idara ya Uzalishaji Mifugo
4. Idara ya Utibabu wa mifugo
5. Idara ya Mazao ya Baharini
6. Ofisi kuu Pemba.

- Katika taarifa ya Wizara Kamati iligundua kwamba, wizara hiyo ina Miradi Mkiuu ifuatayo:

    1. Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu
    2. Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo
    3. Kudhibiti Mafua ya Ndege
    4. Kudhibiti Kichaa cha Mbwa
    5. Kuimarisha Ufugaji wa Samaki
    6. Kupandisha Ngombe kwa Sindano

SEKTA YA UVUVI

1. **Soko la Tumbe.**
   Wakati wa kazi zetu ,Kamati ilitembelea soko la Tumbe lililojengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia chini ya mradi wa MACEMP ambapo tayari limefunguliwa wakati wa sherehe za Mapinduzi zilizopita.

Changamoto iliyopo.

Mkandarasi tayari ameshamaliza kazi yake na ameshakabidhi soko hilo bila ya kutimiza masharti ya mkataba wa ujenzi ambao pia ilijumuisha kuunganishwa kwa umume katika soko hilo. Taarifa zilizogunduliwa na Kamati wakati inatayarisha ripoti hii ni kwamba Serikali imeamua kubeba gharama za kuunganisha umeme katika soko hilo ili litumike huku ikiangalia uwezekano wa kumchukulia hatua za kisheria mkandarasi huyo ambae ameshindwa kutimiza masharti ya mkataba wa ujenzi huo.

Mkataba wa Ujenzi wa soko la Tumbe

Kamati ilielezwa kuwa Mkataba huo wa Ujenzi wa Soko la Tumbe uliingiwa kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Kampuni ya Ujenzi ya Ngogo Engineering Ltd katika mwaka 2011 kwa Shilingi za Kitanzania 1,074,808,177/- na kwa mujibu wa maelezo ya Wizara kazi hii ilitakiwa kukamilika baada ya miezi 7.

Kamati ilielezwa kuwa baada ya kuzama kwa meli ya Mv. Spice Islander tarehe 10/09 / 2011 ambayo ilibeba vifaa vingi vya Kampuni hiyo kwa ajili ya ujenzi huo, makubaliano ya awali juu ya muda wa ujenzi na gharama ilibidi yabadilike na Banki ya Dunia ilikubali kazi hiyo ifanywe kwa gharama ya Shilingi 712,500,000/- badala ya makubaliano ya awali ya Shilingi 1,074,808,177/-.

Hata hivyo kwa kuwa mkataba wa awali uliosainiwa haukubadilishwa , Kamati kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu BLW/K.10/17 VOL.1/100 iliomba ipatiwe maandishi ya kubadilishwa kwa makubaliano hayo ya awali. Kwa masikitiko makubwa sana Kamati ilipokea barua kutoka wizara ya mifugo na Uvuvi licha ya kuikumbusha kwa barua, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya tarehe 25/02/2015 yenye yenye nambari ya kumbukumbu WMU/20/3/21/VOLT ambayo ni tofauti na kielelezo kilichoombwa na Kamati. Kielelezo kilicholetwa ni barua iliyokuwa na kichwa cha habari " ***RE : PROVISSION CONSULTANCES FOR DESIGN AND SUPERVISSION OF THE CONSTRUCTION WORKS OF FISHLANDING SITES AT***

TUMBE IN PEMBA". Kamati iliona kuwa barua hii haihusiani kabisa kuhusiana na suala la kuzama kwa Meli ya MV. Spice Islandeder na kupunguzwa kwa makubaliano ya mwanzo kutoka shilingi 1,074,808,177/- hadi 712,500,000/=.

Aidha meli ya MV. Spice Islandeder ilizama mnamo tarehe 10/9/2015 lakini barua hii ilitoka tarehe tarehe 30 Mei, 2011. Kwa hiyo ni wazi kwamba barua hii ilitoka kabla ya kuzama kwa meli.

Kamati bado inajiuliza jee kupungua kwa gharama za awali sababu ilikuwa ni kuzama kwa meli ya MV. Spice Islander au "**KULIKONI"?**

Ushauri na Maagizo ya Kamati.

- Serikali ihakikishe kwamba mikataba yote inayoingia inafuatwa na kutekelezwa kikamilifu.
- Serikali imchukulie hatua kisheria mkandarasi aliyejenga soko La Tumbe na kulikabidhi bila ya kukamilisha masharti ya mkataba wa ujenzi huo.

2. **Ujenzi wa Soko Malindi**.

   Kamati ilitembelea Eneo linalotarajiwa kujengwa soko jipya la samaki Malindi ambapo ilielezwa kwamba mkataba kwa ajili ya Ujenzi huo tayari umeshasainiwa na ujenzi ulitarajiwa kuanza Mwezi Septemba 2014, na kukamilika 2016 kwa lengo la kuwawezesha wavuvi wetu na wananchi kwa ujumla kupata samaki wenye ubora, usafi na usalama. Ujenzi wa soko la hili ambao ukimalizika utakuwa umegharimu kiasi cha Shilingi za Kitanzani 14,866.500,000/- kwa sasa umesimama, sababu kubwa ya kusimama ujenzi huo ni UNESCO kushindwa kutoa kibali cha ujenzi wa soko hilo kwa madai kwamba mchoro wa jengo hilo hauendani na majengo ya Mji Mkongwe.
   Aidha, Kamati ilielezwa kuwa sababu kuwa khasa ni paa la mchoro huo pamoja na madirisha. Vile vile mchoro huo ulikuwa unafanana na majengo ya Kiarabu lakini UNESCO wametaka ufanane na majengo ya Kiengereza.

   Maagizo ya Kamati

   - Kamati inaigazira Wizara ya Uvuvi na Mifugo kukaa pamoja na Wizara inayohusika na masuala ya Ujenzi pamoja na Mamlka ya Mji Mkongwe ili kujadili suala hili kwa kina na kulitafutia ufumbuzi wa haraka.

   - Wizara kwa kushirikiana na Serikali kuu iangalie uwezekano kwa hali yoyote ile wa kuonana au kuwasiliana na moja kwa moja na UNESCO ili wapewe taarifa za uhakika ni kwanini mpaka sasa hawajatoa kibali cha kuendelea na ujenzi wa soko hilo.

3. **Vikundi vya Ufugaji wa Samaki na Mazao ya Baharini**
   Kamati yetu pia ilibahatika kuwatembelea wafugaji mbali mbali wa samaki na mazao ya Baharini ikiwemo;

1. Wambaa
2. Ufugaji wa Kasa Nungwi
3. Ufugaji wa Chaza Dimani.

Kamati iliridhika na juhudi zinazochukuliwa na kikundi hivyo vya wafugaji katika juhudi zao za uzalishaji wa mifugo na kupambana na hali ngumu ya maisha.

Changamoto za Vikundi

1. Kwa upande wa wafugaji wa samaki wamedai kua Vifaranga vingi vya samaki vinafariki kutokana na ukosefu wa utaalamu wa ufugaji huo. Aidha upatikanaji wa Vifaranga hivyo si vya uhakika na vinawapa usumbufu mkubwa na hawajui watavipata wapi.
2. Vikundi hivyo vya ufugaji wa Samaki, kasa na Chaza Vinahitaji msukumo mkubwa kutoka serikali na wafadhili mbali mbali ili kifikie malengo yaliyojiwekea.
3. Vikundi Vinahitaji utaalamu zaidi wa uzalishaji pamoja na malisho ya mifugo yao.

Maagizo ya Kamati.

- Wizara ya Mifugo na Uvuvi ihakikishe kwamba inawapatia Vifaranga na elimu ya ufugaji kwa vikundi vyote vinavyojishughulisha na Ufugaji wa Samaki, Kasa na Chaza.

4. Kilimo cha Mwani

Kamati ilifika huko Uroa, Wilaya ya Kati pamoja na Dimani Wiaya ya Magharibi na kuonana na wakulima wa mwani wa shehia hizo pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa kilimo cha mwani katika maeneo yao ambapo wameripoti kwamba wanaendelea vizuri na kilimo hicho licha ya changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi.

Changamoto.

- Kipato wanachokipata wakulima hao hakikidhi mahitaji ingawa wanafanya kazi kubwa ya kilimo hicho.
- Bei ya Shilingi 500 kwa kilo moja ya mwani ni ndogo ukilinganisha na kupanda kwa hali ya maisha ikizingatiwa kwamba wakulima hao wanajitegemea wenyewe kwa vifaa.
- Changamoto nyengineinayowapata wakulima hao ni maafa mbali mbali ambayo huwapata hasa kwa kuchomwa na samaki aina ya njenga na kulazimika kutoweza kufanya kazi zao kwa miezi mitatu mpaka minne wala hakuna fidia yeyote wanayoipata.

Maagizo ya Kamati.

- Wizara ifuatilie bei ya mwani duniani kama vile inavyofanya kwa upande wa zao la karafuu ili wakulima wetu waweze kupata bei inayoridhisha na hatimai wapate mpato mazuri ya kazi zao.

SEKTA YA MIFUGO

5. Mashamba ya Mifugo Pangeni.

Eneo la Shamba hili la Pangeni ni la Serikali na linatumika kwa ajili ya Ufugaji wa Ng'ombe, eneo hili kwa sasa lina ng'ombe hamsini (50). Kamati ilipotembelea Shamba hilo ilibaini Changamoto zifuatazo;

- Tatizo la upatikana wa maji jambo ambalo linawafanya Ng'ombe kuwa dhaifu sana.
- Uvamizi wa shamba unaofanywa na baadhi ya wakulima wanaolima karibu ya maeneo na shamba hilo, jambo ambalo limesababisha kuvamiwa shamba hili kwa asilimia kubwa.
- Ukataji miti katika eneo la shamba hilo, jambo ambalo limesababisha miti mingi sasa kupotea.
- Eneo la Shamba halina Hati miliki.

Maagizo ya Kamati

- Wizara ifanye jitihada ili kulitafutia ufumbuzi tatizo la maji katika eneo hilo ili wanyama wanaofugwa katika eneo hilo wapate maji yakutosha.
- Wizara ianze kufatilia maeneo yote yaliyovamiwa na yarudishwe katika mikono ya shamba hilo.
- Serikali ifanye uhakiki juu ya mashamba na maeneo yote ya Serikali ambayo mpaka sasa hayana hati miliki kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi yapatiwe hati miliki kwani kukosekana kwa hati miliki hizo ndio kuna pelekea kuvamiwa kwa mashamba hayo.
- Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Idara ya Misitu waangalie uwezekano wa kuwadhibiti wale wote wanaokata miti katika shamba hilo.

6. Majosho ya Konde, Mjimbini na Kituo cha Mifugo Chamanangwe

Kamati iliutembelea Kituo cha Mifugo na Josho Konde, Mjimbini na Chamanagwe ambavyo kwa sasa vinakabiliwa na Changamoto kadhaa zinazozoretesha utendaji wa vituo hivyo. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

1. Uhaba wa wataalamu
2. uhaba wa vitendea kazi.
3. Kiwango kidogo cha Taaluma kwa wafanyakazi.
4. Uvamizi wa maeneo kwa shughuli za makaazi na kilimo.

Maagizo na maoni ya Kamati

- Wakati Wizara inasuburi kupata hati miliki ya maeneo hayo ni nyema ikachukua hatua za dharura za kuyahami ili kuepusha vitendo vya uvamizi vinavyowea kutokea.

7. Wafugaji Maarufu wa Wilaya ya Mkoani Pemba

Kamati ilimtembelea mfugaji wa Ng,ombe wa maziwa (Bw. Mohammed Jidawi) alianza na ngombe mmoja na hivi sasa anamiliki Ngombe sita wanaotoa maziwa lita 15 kwa siku kwa kila mmoja hukoMjimbini. Bw. Mfugaji huyu ambae licha

ya Ufugaji huo anajishughulisha na kilimo cha aina mbali mbali na ameweza kupiga hatua kubwa za uzalishaji wa Mazao ya mifugo na kilimo.
Aidha Kamati ilifika Makhuduthu, kukagua mradi wa mtambo wa Biogas wa Bw. Hafidh Nassor ambae ameanza shughuli za ufugaji akiwa na ngombe wa maziwa mmoja (1) na hivi sasa anamiliki ngombe sita (6).
Kamati iliridhishwa na juhudi zinazochukulwa na wafugaji hawa na kuwaomba wataalamu wa mifugo na Kilimo kuwa karibu nao kwani ni mfano mzuri wa wazalishaji wetu.

Changamoto

1. Tatizo linalowakabili wafugaji hawa ni upatikanaji wa Madawa , ambapo wamesema upatikanaji wake ni mgumu na pia zinauzwa bei kubwa.
2. Usafiri kwa Maafisa Mifugo- wataalamu wa mifugo hawana usafiri wa uhakikika hivyo wanashindwa kufika kwa wakati pale wanapohitajika kutoa ushauri wa mifugo.
3. Ukosefu wa mbegu bora na sahihi za Mifugo yao.
4. Baadhi ya wakati mbegu za Kupandishia zikiwafikia zinakuwa tayari zimeharibika kutokana na ukosefu wa Sehemu za kuhifadhia na wakati mwengine huhifadhiwa katika chupa za Chai.

Maagizi ya Kamati.

- Wizara ione umuhimu wa kua na Mitungi ya Liquid Nitrogen ambayo ni Portable, ili kuwa na urahisi wa kuwafikia wafugaji walioko vijijini zaidi badala ya kutumia chupa za chai ambapo mara nyingi usafirishaji wa aina hiyo unapelekea mbegu hizo za upandishaji mifugo kuharibika.

Uvuvi wa Bahari Kuu

Kamati imebaini kuwa, Wizara ipo katika maandalizi ya kuanza uvuvu wa Bahari Kuu, miongoni mwa maandalizi hayo ni kuwapeleka vijana wetu huko Tanzania bara kwa ajili ya kujifunza suala zima la uvuvi huo. Pia Kamati imegundua kwamba wizara iko katika hatua za mwisho katika ununuzi wa meli na vifaa vyengine kwa ajili ya Uvuvi huo.

Kutokana na umuhimu wa suala hili, Kamati ilikwenda Bagamoyo Tanzania Bara katia Chuo cha Uvuvi MBEGANI.

Ingawa Kamati haikupata muda wa kutosha katika ziara hiyo , kwani tukiwa safarini kwa huzuni tulipokea taarifa ya Marehemu Salmin Awadh Salmin na kukatisha ziara hiyo, lakini kupitia ziara hii Kamati ilijifunza mambo mengi ya msingi ambayo yanahitaji kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Wizara.

Ushauri na Maagizo ya Kamati

- Wizara iendelee kuwapeleka vijana wetu kujifunza zaidi kwani suala hili linahitaji utaalamu ukilinganisha na uvuvi wa kawaida.

- Wizara iwe makini wakati wa ununuzi wa meli za uvuvi na ihakikishe kwamba meli hizo zitakidhi mahitaji yanayokusudiwa.
- Wakati Wizara inajitayarisha na Uvuvi huu wa Bahari Kuu, ni muhumu kuzingatia ujunzi wa sehemu itakayokuwa na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuhifadhia samaki.
- Kwakuwa jambo hili ni muhimu katika kuinua uchumi wa Zanzibar, Wizara ihakikishe kuwa suala hili linakuwa endelevu kwani rasiliamali kubwa ya nchi ni bahari.

SEHEMU YA TATU

Hitimisho.

Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji , Utalii na Habari ya Baraza la Wawakilishi inawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii, kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa mwaku huu. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Hata hivyo kasoro kubwa iliyogunduliwa na Kamati ni **Upatikanaji wa fedha kutoka serikalini** kwamba umekwamisha kwa kiasi kikubwa malengo na shabaha za Wizara zote mbili hasa katika miradi ya Maendeleo. Vile vile upatikanaji wa fedha za OC pamoja na vitendea kazi, usafiri na malipo ya muda wa ziada wa kazi (over time) navyo vimekuwa virejesha nyuma mwamko na ufanisi wa kazi.

- Kamati inaendelea kuiagiza Serikali kuzipatia Wizara zake fedha za Bajeti kwa wakati na kiwango kilichokubalika.

Aidha Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri.